Kioo cha Lugha, Juz. 24(1), 101-119
Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v24i1.7

Uchunguzi wa Mbinu Zinazosawiri Usihiri katika Bunilizi za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Gloria, V. Kimbi[1]

Ikisiri

Sihiri[2] ni miongoni mwa mbinu inayotumika katika utunzi wa kazi za fasihi ya watoto, bunilizi za Kiswahili za watoto zikiwamo. Ingawa sihiri inatambulika kama nyenzo muhimu katika utunzi wa kazi za watoto, bado mbinu zinazowasilisha usihiri katika kazi za watoto hazijawekwa bayana. Suala hili limesababisha ombwe la maarifa kuhusiana na mbinu zinazowasilisha usihiri, hivyo, mbinu husika kuonekana chapwa katika kazi mbalimbali za fasihi ya watoto hususani katika bunilizi za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Ili kupata maarifa hayo muhimu, makala hii imebainisha na kufafanua mbinu zinazowasilisha usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto ambazo ni: *Sinderela* (Moshi, 1995), *Hadithi ya Morile* (Mariki, 2004) na *Hadithi za Kusisimua* (Mzindakaya, 2005). Data za makala hii zilikusanywa kutoka katika bunilizi tajwa kwa njia ya usomaji na uchambuzi wa matini. Kadhalika, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu katika kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data za makala hii. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto umewasilishwa kupitia mbinu mbalimbali kama vile: mbinu ya ndoto, utamkaji wa neno/maneno, ukiukwaji wa masharti, wimbo na mbinu ya namna au jinsi ya utendaji. Makala hii imeongeza maarifa katika fasihi kupitia bunilizi za Kiswahili za watoto kwa kupanua uga wa uelewa wa kipengele cha sihiri katika fasihi ya watoto hususani fasihi ya Kiswahili ya watoto.

1.0 Utangulizi

Suala la sihiri katika fasihi ya watoto limejadiliwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Mathalani, Fox (2006) anaeleza kuwa sihiri ni mbinu ya utunzi wa kazi za watoto ambayo huwasaidia watoto katika makuzi yao kwani huwawezesha kujua

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: glorykimbi@yahoo.com

[2] Katika makala hii maneno sihiri na usihiri yametumika kwa kubadilishana kurejelea nguvu zinazowezesha kufanyika kwa matendo mbalimbali ambayo kwa hali ya kawaida yasingeweza kutendeka.

masuala mbalimbali ya kimaisha. Nao Subbortsky (2010) na Gavin (2021) wanafafanua kwamba sihiri ni dira katika utunzi wa bunilizi za watoto na hutumika kuwaelekeza watoto namna ya kuishi, kukabiliana na mazingira yanayowazunguka na kuufurahia ulimwengu kwa namna yao. Simpkins (1988), Owen (2012), Cahill (2012) na Nlya (2021) wanabainisha aina mbalimbali za matendo ya kisihiri ambayo ni pamoja na mazingaombwe, uchawi, uganga, miujiza, utabiri, maombi, ushirikina na fantasia. Aidha, Evans, Milanak, Medeirod na Rose (2002) pamoja na Fox (2016) wanaeleza kuwa sihiri ni mbinu muhimu katika ujenzi wa bunilizi za watoto kwani bunilizi za watoto zimetungwa na zinaendelea kutungwa kisihiri. Pamoja na sihiri kuwa suala muhimu katika utunzi wa bunilizi za watoto, bado mbinu za uwasilishaji wa usihiri katika kazi za watoto hazijawekwa bayana. Maelezo hayo yanatokana na ombwe la maarifa kuhusiana na mbinu zinazowasilisha usihiri katika bunilizi za watoto. Kutokana na hayo, makala hii inaweka bayana mbinu mbalimbali zinazowasilisha usihiri katika bunilizi teule za Kiswahili za watoto.

Sihiri katika fasihi ya Kiswahili ya watoto imechunguzwa kwa mawanda finyu. Kwa mfano, wataalamu kama vile Ngugi, Lyimo na Bakize (2019) wamechunguza fantasia katika bunilizi za watoto za Kiswahili. Fantasia ni mtindo wa uwasilishaji wa kazi za kisanaa unaohusisha matukio, wahusika na mandhari ya ulimwengu mwingine, yaani ulimwengu usioonekana wala kufikika na wenye mambo tofauti na ulimwengu halisi (Cahill, 2012; Mahmood, 2020). Aidha, makala hii inatambua fantasia kama miongoni mwa matendo yanayohusisha sihiri. Ingawa wataalamu hawa wanajadili fantasia, hawajaeleza kuhusu mbinu zinazowasilisha fantasia, hivyo, kuacha ombwe la maarifa juu ya mbinu za uwasilishaji wa usihiri katika bunilizi za Kiswahili za watoto. Ili kuweka bayana maarifa hayo muhimu, makala hii imechunguza mbinu zinazosawiri usihiri katika fasihi ya Kiswahili ya watoto kwa kutumia mifano kutoka katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili za watoto.

2.0 Nadharia ya Uhalisiajabu

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu iliyoasisiwa na Franz Roh mwaka 1925 aliyehusisha uhalisiajabu na masuala ya sanaa ya uchoraji (Anne, 1994; Cooper, 1998; Bowers, 2004; Faris, 2004). Anne (1994) anaeleza kuwa uchoraji alioujadili Franz Roh ulilenga kufichua siri zilizoko kwenye maisha ya kila siku bila kupinga moja kwa moja masuala halisi. Aidha, nadharia hii ilihusishwa kwa mara ya kwanza na fasihi ya Amerika ya Kusini na Gabriel Garcia mwaka 1927. Kipindi hiki kinajulikana kama awamu ya kwanza ya matumizi ya Nadharia ya Uhalisiajabu (Cooper, 1998). Nadharia hii iliendelea kutumika huko Amerika ya Kati miaka ya 1940, kipindi ambacho kinajulikana kama awamu wa pili ya matumizi ya Nadharia ya Uhalisiajabu (Bowers, 2004). Bowers anafafanua zaidi kuwa awamu ya tatu ya matumizi ya Nadharia ya Uhalisiajabu ilianza huko Amerika ya Kaskazini na maeneo mengine duniani miaka ya 1960. Aidha,

nadharia hii imekuwa ikitumika katika kazi mbalimbali za kifasihi (Anne, 1994; Faris, 2004). Anne (1994) anaeleza kuwa uhalisiajabu katika kazi za sanaa hushughulika na kazi zinazoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia. Naye Cooper (1998) anabainisha kuwa uhalisiajabu huufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na vile ilivyozoeleka. Bowers (2004) kwa upande wake anaainisha misingi mitatu ya Nadharia ya Uhalisiajabu ambayo ni: wakati na mahali kuwa na uhusiano wa kiduara, matokeo ya kiuhalisiajabu kushangaza, kuduwaza na wakati mwingine kuogofya pamoja na kazi za kifasihi kuhusisha sanaa jadia kama vile visasili na visakale katika kufafanua masuala mbalimbali ya maisha. Aidha, Faris (2004) anabainisha misingi mitatu ya Nadharia ya Uhalisiajabu ambayo ni: mosi, matendo ya ajabu na halisi huungana katika kutekeleza wajibu maalumu katika jamii. Pili, matendo ya ajabu husababisha ukosefu wa utulivu wa kisaikolojia katika kuelewa mpaka kati ya uajabu na uhalisia. Tatu, wakati na mahali huwa na uhusiano wa kiduara.

Baada ya kufafanua misingi ya Nadharia ya Uhalisiajabu iliyobainishwa na wataalamu tajwa hapo juu, utafiti wa makala hii umebaini kuwa misingi husika inaingiliana sana. Kutokana na maelezo hayo, utafiti huu umeunganisha misingi yote iliyobainishwa na wataalamu tajwa hapo juu kwa kuepuka uradidi kisha kuitumia kama mwongozo wa utafiti huu. Misingi hiyo ni kama ifuatavyo: mosi, uhalisiajabu hueleza masuala halisi na kuyahusisha na yale yasiyo halisi katika kutekeleza wajibu fulani. Pili, uhalisiajabu husababisha ukosefu wa utulivu wa kisaikolojia katika kuelewa mpaka kati ya uajabu na uhalisia. Tatu, uhalisiajabu husaidia kuvunjwa kwa mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa wakati wa kuelezea kazi za kifasihi na kisanaa. Nne, uhalisiajabu huruhusu kazi za kifasihi kuhusisha sanaa jadia kama vile visasili na visakale katika kufafanua masuala mbalimbali ya maisha. Tano, uhalisiajabu huruhusu matukio katika kazi ya kifasihi kukosa mfuatano wa kimantiki. Ingawa Nadharia hii ina misingi mitano kama ilivyobainishwa hapo juu, ukusanyaji, uwasilishaji na uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na msingi mmoja kati ya mitano. Msingi uliotumika ni ule unaoeleza kuwa uhalisiajabu hueleza masuala halisi na kuyahusisha na yale yasiyo halisi katika kutekeleza wajibu fulani. Msingi huu una maana kuwa uhalisiajabu huhusisha matendo ya kawaida yanayotoa matokeo yasiyo ya kawaida ambayo hayajazoeleka katika jamii. Msingi huu umeongoza utafiti katika kuwasilisha na kuchambua data zilizopatikana kwa kusoma bunilizi teule za makala hii.

3.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zimepatikana kupitia mbinu ya usampulishaji lengwa. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti katika kuteua bunilizi teule za utafiti. Mtafiti alikusanya bunilizi tano za fasihi ya Kiswahili ya watoto alizozipata maktabani na kuzisoma. Baada ya zoezi la usomaji, baadhi ya bunilizi zilikosa sifa ya kuwa sampuli ya utafiti huu. Hivyo, kati ya bunilizi tano, bunilizi mbili zilikosa sifa ya kuwa

sehemu ya utafiti huu kwa sababu hazikuhusisha matendo ya kisihiri. Bunilizi tatu zilizobaki zilikidhi vigezo vya kuwa sampuli ya utafiti huu ambazo ni *Sinderela* (Moshi, 1995), *Hadithi ya Morile* (Mariki, 2004) na *Hadithi za Kusisimua* (Mzindakaya, 2005). Kwa kuwa makala hii ilihitaji bunilizi zilizoundwa kisihiri, itoshe kusema kuwa bunilizi teule ndizo bunilizi lengwa na faafu zilizotumika kama sampuli ya makala hii. Mtafiti alipata bunilizi lengwa kwa kutumia mbinu ya usomaji matini. Pia, data za makala hii zimechambuliwa kitaamuli. Bunilizi hizi zimemsaidia mwandishi wa makala hii kufafanua mbinu zinazowasilisha usihiri wa matendo mbalimbali yaliyounda bunilizi husika.

4.0 Muhtasari wa Bunilizi Teule

Makala hii imechunguza mbinu zinazosawiri usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Bunilizi hizo ni *Sinderela*, *Hadithi ya Morile* na *Hadithi za Kusisimua*. *Sinderela* ni bunilizi iliyoandikwa na Riet Moshi mwaka 1995. Bunilizi hii inahusu maisha ya msichana aitwaye Sinderela aliyekuwa akiishi na mama wa kambo aliyemtesa sana baada ya wazazi wake kufariki. Bunilizi hii inamwonesha Sinderela akisaidiwa na bibi yake marehemu aliyefika kwenye sherehe ya mfalme na kuonana na mtoto wa mfalme kisihiri. Baada ya sherehe kuisha, mtoto wa mfalme alimpenda Sindelela na kumuoa. Maisha ya Sindelela yalibadilika na kuwa ya furaha kwani aliepukana na chuki, dhihaka na mateso aliyopewa na mama yake wa kambo.

Pia, *Hadithi ya Morile* ni bunilizi iliyoandikwa na Freda Mariki mwaka 2004. Bunilizi hii inasimulia maisha ya mtoto aliyejulikana kwa jina la Morile. Bunilizi inaonesha namna Morile alivyokutana na kiazi chenye umbo la mtoto wakati akimsaidia mama yake kuchimba viazi. Mwandishi anaeleza namna Morile alivyokihifadhi kiazi hicho pangoni pamoja na mabadiliko ya kiazi kuwa mtoto ambaye Morile alimpa jina la Kitonga. Vilevile, bunilizi hii inawaonesha wazazi wa Morile walivyomchukua Kitonga kutoka pangoni na kumficha. Hivyo, Morile alikasirika na kuamua kupaa mawinguni kisihiri kwa lengo la kumuuliza aliyempa mtoto (Kitonga) juu ya mambo yaliyomtokea. Aidha, bunilizi hii inaeleza namna Morile alivyoyeyuka na kutoweka kabisa baada ya kula nyama aliyokatazwa.

Aidha, *Hadithi za Kusisimua,* hii ni bunilizi iliyoundwa na hadithi ndogondogo kadhaa zinazoelezea masuala mbalimbali iliyoandikwa na Chrisant Mzindakaya mwaka (2005). Miongoni mwa hadithi zinazounda bunilizi hii ni pamoja na hadithi inayohusu kijana aliyeitwa Furahisha. Hadithi hii inaeleza namna Furahisha alivyotokewa na jitu la kutisha ndotoni. Jitu hilo lilimwelekeza Furahisha namna ya kukutana katika maisha halisi na msichana aliyemwona ndotoni na kumpenda. Aidha, hadithi nyingine zinazounda bunilizi hii ni pamoja na hadithi ya "Kijana Jasiri", “Simba Wazi”, “Chui Alivyopata Ukali” pamoja na “Hadithi ya Kilio cha Zumya”. Hadithi zote kwa pamoja zinakamilisha bunilizi inayojulikana kwa jina la *Hadithi za Kusisimua*. Aidha, utafiti wa makala hii ulirejelea hadithi tatu tu kati ya hadithi kadhaa zinazounda bunilizi ya *Hadithi za*

Kusisimua. Hadithi husika ni pamoja na: "Hadithi ya Kijana Furahisha", hadithi ya "Kijana Shujaa" pamoja na hadithi ya "Simba Wazi".

5.0 Mbinu Zilizotumika Kuwasilisha Usihiri katika Bunilizi za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Usihiri katika bunilizi za fasihi ya Kiswahili ya watoto umewasilishwa kupitia mbinu mbalimbali. Mbinu zilizobainika katika bunilizi teule ni zifuatazo:

5.1 Mbinu ya Ndoto

Ndoto ni hali inayotokea kwa mtu anapokuwa katika usingizi mzito, hivyo, kusababisha mtu huyo kufanya mambo ya kawaida au yasiyo ya kawaida kana kwamba yupo katika mazingira halisi (Salsich, 2012). Maelezo ya Salsich yanaonesha kwamba ili mtu aote ni lazima awe amesinzia. Aidha, utafiti huu unatambua ndoto kama maono mbalimbali ayaonayo mtu wakati akiwa amelala bila kuzingatia wakati. Hivyo, ndoto huweza kutokea mchana au usiku wakati mtu amelala. Utafiti huu umebaini kuwa ndoto ni miongoni mwa mbinu iliyotumiwa na waandishi wa bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto katika kuwasilisha usihiri. Kupitia mbinu ya ndoto, usihiri unaosawiri maisha halisi ya jamii zilizolengwa na watunzi wa bunilizi husika uliwasilishwa. Kwa mfano, bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* imeeleza namna Furahisha alivyopewa maelekezo ya namna ya kumpata mke aliyemtaka kutoka kwa jitu la kutisha kupitia ndoto. Kiuhalisia, ndoto na mke ni masuala mawili yasiyo na ukuruba. Tofauti na hayo, ndoto imetumika kisihiri kumkutanisha Furahisha na mwanamke mrembo asiyemfahamu. Data kutoka bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* inadhihirisha haya pale mwandishi anapoeleza:

> Furahisha alikuwa ndotoni. Lile jitu la kutisha lilimtokea. Likasema, "Ukishakata kidole chako cha mwisho cha mkono wa kushoto, ikinge damu ya kwanza katika chungu kidogo. Kumbuka kuwa mwangalifu ili damu ya kwanza isidondoke chini". … "Furahisha aliinua kidole cha mkono wake wa kushoto kikiwa juu ya chungu kidogo. Alitoa wembe na kukata kipande cha kidole chake kidogo. Kwa mshtuko na maumivu ile damu ya kwanza ilichuruzika chini lakini nyingine akaikinga kwenye chungu. Kufumba na kufumbua likatokea joka kubwa la kutisha. Lakini katika usawa wa chungu alisimama yule msichana mzuri aliyemwona ndotoni. "Sasa ndoto yangu imekuwa kweli". Furahisha alisema (Mzindakaya, 2005: 5-6).

Dondoo hilo limeeleza jinsi Furahisha alivyoonana na jitu kupitia ndoto. Pia, linadhirihisha maelekezo ya jitu kwa Furahisha juu ya mbinu za kumpata mke aliyemtaka. Maelezo hayo yanaonesha njia alizotumia jitu kumwelekeza Furahisha namna ya kukutana na mwanamke aliyempenda. Aidha, masuala haya yameelezwa kwa kuongozwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisiajabu unaoeleza kuwa uhalisiajabu hueleza masuala halisi na kuyahusisha na yale yasiyo halisi katika

kuwasilisha suala fulani. Data katika dondoo hapo juu linathibitisha kuwa watu huelekezwa namna ya kufanya masuala mbalimbali katika maisha ya kila siku. Hivyo, maelekezo kama suala halisi yamefungamanishwa na ndoto kama suala lisilo halisi kusababisha muungano au kuonana kwa Furahisha na mwanamke aliyempenda. Kutokana na mfungamano huo, Furahisha aliweza kukutana na mwanamke aliyemwona na kumpenda ndotoni katika mazingira halisi. Ndoto hufungamana na sihiri za wahenga katika kuhakikisha usalama wa kizazi hadi kizazi kwa masuala yote ya kijamii (Tempels, 1957). Wahenga huwasaidia watu wa nasaba zao kutatua matatizo mbalimbali yanayowasibu (Florian, 2016). Lawrence (2015) anaeleza kwamba sihiri hufungamana na roho za siri zenye nguvu katika kukamilisha suala fulani zuri au baya. Maelezo ya Lawrence, yanathibitisha kwamba kulikuwa na roho ya siri yenye nguvu iliyompa jitu uwezo wa kukutana na Furahisha kupitia ndoto.

Pia, data inaonesha kuwa Furahisha alipaswa kukata kidole chake cha mkono na kukinga damu kwa kutumia chungu. Weismantel (2004) anaeleza kuwa chungu ni kifaa cha kupikia kilichotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi. Weismantel anafafanua kuwa chungu hubeba dhana ya utamaduni wa asili ya Kiafrika, moja ya urithi kutoka kwa wazee wetu wa kale. Aidha, chungu huwa na faida lukuki katika mapishi na afya. Husaidia kuhifadhi virutubisho vya vyakula wakati wa mapishi na kuongeza ladha ya chakula. Zaidi ya hayo, jamii nyingi za Kiafrika hutumia chungu katika miviga, kwa mfano, matambiko na uchawi (Kimaryo, 2008). Kwa kuwa Furahisha alihitaji kumuoa msichana ambaye ni wa asili ya utamaduni wake, hakuna shaka kuwa chungu kilitumika kwa kuwa ni kifaa cha asili ambacho hutumika kutekeleza masuala mbalimbali ya kiutamaduni. Vilevile, Furahisha alipaswa kutoa damu kwa sababu mara nyingi damu hutumika katika maagano kupitia matambiko ya jamii mbalimbali. Kwa mfano, katika jamii ya Wachaga watu hutumia damu ya wanyama kumkaribisha mtoto mpya katika familia (Brock-Utne, 2018). Brock-Utne anafafanua zaidi kuwa damu husika hutokana na wanyama hasa mbuzi. Masuala haya hufanyika ili kukamilisha matendo fulani ya kiutamaduni. Hivyo, sihiri humwezesha mtu kukamilisha malengo yake binafsi na hata ya jamii nzima (Cahill, 2012).

Fish (2016) anaeleza kuwa ili kukamilika kwa tendo la kisihiri ni lazima kufuatwa kwa masharti mbalimbali. Masharti hayo hutumiwa kama kipimo cha kutaka kuhakikisha mahitaji ya mtu kwa sihiri anayoihitaji. Kutokana na hayo, data katika dondoo tajwa hapo juu inaonesha kuwa Furahisha alielekezwa kukata kidole chake kidogo cha mkono, kukinga damu kutoka katika jeraha atakalopata katika kidole chake na kuhakikisha kuwa damu haidondoki chini kama masharti ya kukamilisha tambiko husika. Ukiukaji wa sharti mojawapo la kisihiri huweza kusababisha matokeo hasi kwa msihiri (Kohnert, 1996). Data inaonesha kuwa Furahisha kama msihiri alishindwa kukinga damu yote iliyotoka kidoleni katika chungu kutokana na maumivu aliyoyapata baada ya kukata kidole, hivyo, kiasi kidogo cha damu kilidondoka chini na kusababisha kutokea kwa joka kubwa

sehemu iliyodondokea damu. Joka husika lilikuja kama adhabu kwa Furahisha kwa kushindwa kutimiza masharti ya jitu. Suala hili linaogofya na linashangaza sana. Pia, linatoa angalizo la kuwa makini wakati wa kutekeleza masuala mbalimbali katika maisha. Vilevile, sihiri huambatana na roho za siri zenye nguvu ambazo huonekana kupitia maumbo ya viumbe wa kutisha. Viumbe hao huwa marafiki na msihiri ili iwe rahisi kukamilisha walichokusudia (Abercromby, 1990). Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa jitu lililomtokea Furahisha katika ndoto lilitumika kuwakilisha roho zenye nguvu zilizomsaidia Furahisha kutimiza azma yake. Suala hili linathibitisha usihiri wa maelekezo ya jitu kwa Furahisha kupitia ndoto.

5.2 Mbinu ya Utamkaji wa Neno/Maneno

Hii ni mbinu nyingine iliyotumika kuwasilisha usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, neno ni kipashio cha usemaji ambacho hujengwa na mwanadamu au mkururo wa sauti zilizopangika kisilabi ambazo hutambuliwa na wasemaji wa lugha husika kuwa kitu kimoja chenye maana mahususi (TUKI, 2004). Kutokana na ufafanuzi huo juu ya dhana ya neno, makala hii imerejelea neno kama tamko mojawapo miongoni mwa mengi ambayo mtu huyatamka katika mchakato wa mazungumzo. Neno huweza kusimama peke yake au kusindikizwa na maneno mengine kadhaa ili kuleta maana iliyokusudiwa. Aidha, makala hii imebaini kuwa kuna namna tofautitofauti za utamkaji wa maneno katika kuwasilisha matendo ya kisihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto kama yafuatayo:

5.2.1 Utamkaji wa Maneno Elekezi

Makala hii imebaini kuwa maneno elekezi ni miongoni mwa mbinu zilizowasilisha usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, BAKITA (2015) linaeleza kuwa uelekezi ni maelekezo ya namna au jinsi ya kufanya jambo ambayo mtu hupewa. Kutokana na fasili hiyo, ni wazi kwamba maneno elekezi ni maneno ya maelekezo apewayo mtu juu ya namna ya kufanya jambo fulani. Mbinu ya utamkaji wa maneno elekezi imetumika katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali. Mathalani, katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* maneno elekezi yametumiwa na mzee Ali kwa mwanawe Ali-Simba alipomtokea katikati ya pori wakati Ali-Simba akiwa safarini kutoka katika kijiji chao kuelekea katika nchi ya Mfalme Daudi. Maneno yaliyobainishwa katika bunilizi teule yameoneshwa katika data ifuatayo:

> Mzee Ali anamwambia Ali-Simba; “Funga macho mwanangu,” Ali-Simba akafunga macho. Mzee Ali akamwambia tena Ali- Simba: “Fungua macho” Ali- Simba alifungua macho na kujikuta yuko katikati ya mji mkuu wa nchi ya Mfalme Daudi alipokuwa akienda kwa ajili ya kupambana na joka lililowatesa watu wa nchi hiyo kwa muda mrefu (Mzindakaya, 2005: 30).

Dondoo hilo linamuonesha mzee Ali akitamka maneno elekezi “funga na fungua” kuwasilisha usihiri wa kutoka eneo moja walilokuwa (katikati ya pori) kisha kuingia katika mji mkuu wa nchi ya mfalme Daudi. Suala hili lina maana kuwa, kuna jambo la siri ambalo mzee Ali alitaka kufanya bila ya Ali-Simba kuona, ndiyo maana alimwelekeza kufunga macho ili alikamilishe. Baada ya kukamilisha jambo alilolikusudia, alimwelekeza kufungua macho. Barley (2006) anaeleza kuwa usiri humwezesha msihiri kutimiza masuala fulani ambayo si halisi wala hayajazoeleka katika jamii. Imebainika katika utafiti huu kuwa mzee Ali alimtaka Ali-Simba afunge macho ili asiweze kuona aliyokuwa akifanya. Pia, utafiti huu umebaini kuwa maneno elekezi yaliyohamisha watu kutoka katikati ya pori na kuwaingiza katika mji mkuu wa nchi yalitoka kwa mzee Ali kwenda kwa mwanawe Ali-Simba. Suala hili linamaanisha kwamba maneno elekezi huweza kuambatana na sihiri kutoka kwa wahenga ambao huhakikisha usalama wa watu wake kizazi hata kizazi (Mbiti, 1969). Aidha, watu hutumia sihiri katika mapigano (vita) ili kuwawezesha wapiganaji kuwa na uwezo zaidi kivita, hivyo, kupambana na wapinzani wao (Mulokozi, 2002). Makala hii imebaini kuwa Mzee Ali alitumia sihiri kumlinda Ali-Simba asipate madhara kutoka kwa wanyama wakali waliokuwa wanatumia pori alilokuwa anapita Ali-Simba kama makazi yao na kumfikisha salama katika nchi ya mfalme Daudi.

Kadhalika, msingi wa Nadharia ya Uhalisiajabu unaoeleza kuwa masuala halisi huhusishwa na yale yasiyo halisi katika kuwasilisha suala fulani umetumika katika kufafanua hoja hii. Suala hili linatokana na sababu kwamba, maneno elekezi “funga na fungua” ni maneno ya utendeshi yaliyozoeleka katika jamii kwa sababu hutumiwa mara kwa mara na wanajamii katika mazungumzo yao. Masuala yasiyo halisi ni maneno elekezi kuhamisha watu kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Kuhusianishwa kwa masuala haya mawili, yaani maneno elekezi na uhamisho wa watu kutoka eneo moja kwenda jingine kunazalisha tendo la kisihiri. Suala hili linatokana na sababu kwamba matokeo ya maneno elekezi kama yalivyotumika katika data hapo juu hayahusiani kabisa na kazi ya jicho kiuhalisia ambayo ni kuona pale linapofunguliwa na kutokuona linapofungwa. Pia, macho ndiyo dira ya mwili wa binadamu kwa sababu humwezesha kuona vitu mbalimbali katika uso wa dunia (Slaughter, Heron, Jenkins, Tilse, Müller na Liebermann, 2004). Hivyo, kulingana na data ya makala hii, maneno “funga” na “fungua” macho yametumika kisihiri kama chombo cha usafiri.

5.2.2 Utamkaji wa Maneno ya Maombi

Maombi ni mahitaji ya mtu yanayopelekwa kwa kiongozi au kwa mtu mwenye madaraka kwa lengo la kutimizwa (BAKITA, 2022). Kutokana na maelezo hayo, maneno ya maombi ni maneno yanayoonesha uhitaji wa msaada kutoka kwa mtu mwenye mamlaka na uwezo wa kutatua shida mbalimbali za watu. Makala hii imebaini kuwapo kwa matumizi ya mbinu hii katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Kwa mfano, katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua*

imeelezwa namna Simba-Wazi alivyopata mahitaji yake mbalimbali kama utajiri, kujibadilisha muonekano na kuwa simba, jua, mwezi na wingu kwa kutumia maneno ya maombi. Simba-Wazi aliiomba pete aliyokuwa nayo impatie kile alichokitaka kwa kutamka maneno ya maombi ya vitu au masuala aliyoyahitaji. Lengo la pete lilikuwa kubadilisha maisha ya Simba-Wazi kutoka katika hali ya umaskini kwa kumpatia utajiri. Data kutoka katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* inathibitisha haya pale Simba-Wazi anapoeleza:

> "Pete naomba niwe Tajiri". Palepale kufumba na kufumbua Simba-Wazi akawa tajiri. Pori lililokuwa pale lilibadilika na kuwa jumba kubwa sana la kifahari (Mzindakaya, 2005: 52).

Dondoo hilo linaonesha namna Simba-Wazi alivyotoka katika hali ya umaskini na kuwa tajiri kwa kutamka maneno ya kuomba kile alichokitamani. Aidha, masuala mawili yamebainika kutokana na data tajwa hapo juu. Kwanza, ni suala la Simba-Wazi kuiomba pete impatie utajiri na akawa tajiri. Kwa kawaida, pete haiwezi kumfanya mtu kuwa tajiri. Suala hili linatokana na sababu kwamba pete ni pambo linalovaliwa na watu kwenye vidole vya mkono (Kozlov, 2003). Kutokana na maelezo hayo, pete si kiumbe hai, hivyo, hakina uwezo wa kufanya jambo lolote. Kitendo cha pete kumpatia mtu utajiri kinamaanisha kuwa pete husika ilikuwa na nguvu za siri zipitazo zile halisi ambazo ndizo zinazorejelewa katika utafiti huu kama sihiri. Samwel (2012) anaeleza kuwa nguvu za sihiri hutoka kwa Mungu, miungu, majini na hata maumbile asilia ya ulimwengu. Kutokana na hayo, utafiti huu umebaini kuwa bunilizi teule ya makala hii haijaeleza bayana chanzo cha sihiri ya pete iliyomwezesha Simba-Wazi kuondoka katika hali ya umaskini na kuwa tajiri. Maelezo haya yanayapa maombi sifa njema ya kufanikisha masuala mbalimbali ambayo watu huomba. Varelius (2013) anaeleza kuwa maombi huweza kusababisha matokeo chanya au hasi. Kwa mantiki hiyo, si lazima maombi yampatie mtu kile alichokiomba. Wakati mwingine huweza kumpatia kinyume na alichoomba.

Suala la pili, lililobainika katika dondoo la hoja hii ni pori alilokuwa amekaa Simba-Wazi kubadilika na kuwa jumba kubwa la kifahari. Pori ni eneo au sehemu yenye miti mingi midogo kwa mikubwa, wanyama na wadudu mbalimbali nje na makazi ya binadamu (Haward, 2003). Hivyo, makala hii imebaini kuwa pori limetumika kumaanisha eneo lenye uoto mwingi. Pia, pori limehusianishwa na jumba la kifahari kwa sababu jumba husika hupambwa kwa samani nyingi na nzuri kama pori linavyokusanya uoto wa aina mbalimbali ambao kwa pamoja huzalisha dhana ya pori. Maelezo haya yamepatikana kwa kuongozwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisiajabu unaoeleza kuwa masuala halisi huhusishwa na yale yasiyo halisi katika kuwasilisha suala fulani. Kutokana na data ya hoja hii, masuala halisi ni pete na pori. Masuala yasiyo halisi ni utajiri unaotokana na pete pamoja na pori kuwa jumba la kifahari. Aidha, kiuhalisia pete haiwezi kumpatia mtu utajiri. Pia, pori haliwezi kubadilika na kuwa jumba kubwa la kifahari. Ili

nyumba iwepo ni lazima ijengwe (Sommer, 2001). Tofauti kabisa na maelezo ya Sommer (2001), Kozlov (2003) na Haward (2003), makala hii inaonesha kuwa pete ilimpatia Simba-Wazi utajiri na pori lilibadilika kuwa jumba kubwa bila kujengwa. Masuala haya yanathibitisha usihiri uliokuwa ndani ya pete aliyokuwa nayo Simba-Wazi. Zuesse (1975) anaeleza kuwa sihiri hutoka kwa roho zenye nguvu zisizoonekana ambazo huwa na nguvu nzuri na mbaya. Kwa upande wa data ya hoja hii, nguvu za sihiri zilizokuwa ndani ya pete zilikuwa nzuri, ndio maana zilimpatia Simba-Wazi kila alilolihitaji. Pia, makala hii imebaini kuwa maneno ya maombi huweza hutumika kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali kama yalivyoelezwa katika ufafanuzi wa hoja ya makala hii.

5.3 Ukiukaji wa Masharti

Ukiukaji wa masharti ni miongoni mwa mbinu zinazowasilisha usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Ukiukaji ni hali ya kwenda kinyume na kanuni au taratibu zilizowekwa juu ya masuala, vitu na watu mbalimbali (TUKI, 2014). Kwa kurejelea fasili hiyo, ni wazi kuwa ukiukaji wa masharti ni kwenda kinyume na maelekezo yaliyotolewa kuhusiana na suala fulani. Katika makala hii mbinu ya ukiukaji wa masharti ilitumiwa na Morile katika bunilizi ya *Hadithi ya Morile* kwani alikula nyama ya fahali aliyemwambia kuwa asile nyama yake wakati atakapochinjwa. Aidha, imebainika kuwa Morile alikula nyama husika baada ya mama yake kuweka katika chakula chake. Data ifuatayo inaonesha Morile akimlaumu mama yake:

> "Mama umenipa nyama ya yule fahali aliyenikataza nisimle atakapochinjwa. … Basi kwaherini. Namfuata fahali wangu". Baada ya kutamka maneno hayo Morile aliyeyuka na kupotea kabisa (Mariki, 2004: 21).

Dondoo hilo linadhirihisha kuwa fahali alimkataza Morile kula nyama yake atakapochinjwa. TUKI (2004) inaeleza kuwa fahali ni ng'ombe dume. Suala hili lina maana kuwa fahali wa Morile hakuwa kama mafahali wa kawaida kwa sababu alifanya mambo ambayo ng'ombe dume wengine hawawezi kufanya. Annus (2015) anasema kuwa miungu pamoja na nguvu kutoka kuzimu huwasiliana na binadamu kupitia viumbe mbalimbali na wakati mwingine hupitia kwa binadamu wengine. Tofauti na maelezo ya Annus, chanzo cha sihiri aliyokuwa nayo fahali wa Morile hakijawekwa bayana. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa Morile na fahali ni viumbe halisi wanaopatikana ulimwenguni. Suala lisilo halisi ni Morile kuyeyuka baada ya kula kipande cha nyama ya fahali. Kimsingi, fahali hana sifa ya kutoa masharti ambayo yanatoa matokeo halisi ya kuyeyuka kwa mlaji wa nyama yake. Kutokana na hayo, mtu kuyeyuka baada ya kula nyama ya fahali ni tendo la kisihiri. Dimmock na Fisher (2017) wanaeleza kuwa ili kukamilisha suala la kisihiri ni lazima msihiri kutimiza masharti aliyopewa (Zuesse, 1975). Kanuni na taratibu za kukamilisha suala la kisihiri zinapaswa kufuatwa ili msihiri asipate

matokeo yaliyo kinyume na matarajio yake (Capers, 2006). Maelezo hayo yanathibitisha kuwa ukiukaji wa masharti ya kisihiri husababisha athari mbaya. Sharma (2018). anaeleza kuwa ili kukamilisha suala la kisihiri ni lazima msihiri atimize masharti aliyopewa. Sharma anaeleza zaidi kuwa masharti ya sihiri yasipozingatiwa, msihiri hawezi kupata matokeo anayoyatarajia. Kutokana na data ya hoja hii, Morile alikiuka masharti aliyopewa na fahali, hivyo, alipata athari mbaya ya kuyeyuka na kupotea kabisa katika uso wa dunia. Kuyeyuka ni kitendo cha dutu mgando kubadilika na kuingia katika hali ya kitowevu (Pfeffer, 2011). Mtaalamu huyu anatoa mfano wa vitu vinavyoweza kuyeyuka kama vile plastiki, chuma na hata barafu. Kutokana na maelezo hayo, binadamu hawezi kuyeyuka. Aidha, matokeo ya makala hii yanapingana na maelezo ya Pfeffer. Suala hili limetokana na sababu kuwa makala hii imeonesha namna binadamu alivyoyeyuka na kupotea kabisa. Binadamu huyo ambaye ni Morile aliyeyuka kwa sababu alikiuka masharti ya utekelezaji wa sihiri yake.

5.4 Mbinu ya Wimbo

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kwamba wimbo ni utungaji wa kimuziki wenye lengo la kutendwa kwa kutumia sauti ya binadamu. Kutokana na ufafanuzi huo, makala hii inarejelea wimbo kama mpangilio wa maneno wenye kufuata mapigo fulani ya kimuziki. Imebainika katika makala hii kuwa wimbo elekezi umetumika kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Wimbo husika ulilenga kutoa maelekezo kwa mtu juu ya namna ya kufanya jambo. Mtu husika hupaswa kutekeleza yale anayoelekezwa na wimbo ili suala la kisihiri lililokusudiwa na wimbo unaoimbwa liweze kukamilika (Fukkink na Glopper, 1998). Aidha, makala hii kupitia bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto imeonesha namna wimbo ulivyotumika kuelekeza kufanyika kwa matendo mbalimbali ya kisihiri. Matendo husika ya kisihiri hudhihirika wakati wimbo ukiimbwa au mara baada ya wimbo kukamilika kuimbwa. Kwa mfano, katika bunilizi ya *Hadithi ya Morile,* Morile aliimba wimbo alipokuwa anataka kupaa kuelekea kwa mungu mwezi kumuuliza sababu za yeye kumpatia mtoto mzuri aliyetokana na kiazi kitamu. Morile anaimba kama ifuatavyo:

> Morile napanda, napanda juu,
> Kiti paa, kuelekea mawinguni,
> Mpandishe Morile mpaka mawinguni. …
> (Mariki, 2004: 7)

Dondoo hilo linaonesha wimbo ukielekeza kiti kupaa kuelekea juu mawinguni. Morile aliimba wimbo wenye maneno “Kiti paa, kuelekea mawinguni” kueleza namna kiti kilivyoelekezwa kupaa kutoka ardhini kikiwa kimekaliwa na Morile kuelekea mawinguni. Akima (1982) anaeleza kuwa nyimbo ni mbinu za awali kabisa zilizotumika kujilinda dhidi ya hatari pamoja na ulimwengu usioonekana.

Anafafanua zaidi kuwa nyimbo zilitumika kuomba msaada roho zenye nguvu zisizoonekana katika kukamilisha suala fulani. Roho husika humsaidia msihiri kufanikisha matamanio yake pamoja na kujilinda dhidi ya maadui. Abercromby (1990) kwa upande wake anaeleza kuwa nyimbo hutumika kuomba msaada roho zenye nguvu zisizoonekana katika kukamilisha suala fulani. Aidha, Abercromby anafafanua zaidi kuwa nyimbo hutumika kutanguliza tendo analotaka kutenda msihiri. Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa wimbo wa Morile ulitumika kutambulisha kile alichotaka kukifanya.

Naye Bradley (1997) anaeleza kuwa wimbo ni silaha muhimu katika kukamilisha tendo la kisihiri. Suala hili linatokana na sababu kwamba wimbo hutumika kuomba ulinzi kutoka kwa roho zenye nguvu, kuonesha uasili wa jambo fulani na hata kuboresha palipoharibika. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa wimbo wa Morile ulilenga kuelekeza kiti kupaa kutoka ardhini kumpandisha Morile kuelekea mawinguni. Aidha, data inaonesha kuwa Morile alitumia kiti ambacho kilimnyanyua kutoka ardhini hadi mawinguni. Kadiri Morile alivyoimba ndivyo kiti kilivyozidi kupaa na hatimaye alitokomea kabisa mawinguni. Kiti ni kifaa kilichoundwa kwa lengo la kukaliwa (BAKITA, 2022), hivyo, siyo chombo cha usafiri. Aidha, mtu kutumia kiti kupaa angani ni kitendo kisicho cha kawaida kwa sababu kifaa halisi kwa usafiri wa angani ni ndege (Meilinger, 2000). Kwa mantiki hiyo, binadamu hana uwezo wa kupaa. Kitendo cha Morile kupaa kinathibitisha kuwa wimbo alioimba Morile ulikuwa na nguvu zipitazo zile za binadamu wa kawaida. Vilevile, tendo la Morile kuimba wimbo uliowezesha kiti kupaa ni la kisihiri. Matokeo haya yamepatikana kwa kuongozwa na msingi wa Nadharia ya Uhalisiajabu unaoeleza kuwa masuala halisi huhusianishwa na yale yasiyo halisi katika kutekeleza suala fulani. Aidha, wimbo na kiti ni masuala halisi yanayopatikana katika mazingira yanayomzunguka mwanadamu. Suala linalokiuka uhalisia ni wimbo kuelekeza kiti kupaa. Kuungana kwa matendo halisi pamoja na yasiyo halisi kunazalisha tendo la kustaajabisha la wimbo kuelekeza kiti kupaa kikiwa kimekaliwa na mtu. Tendo husika huwezekana kutokana na uwepo wa nguvu ya siri ipitayo zile za kibinadamu. Nguvu husika ndizo zinazotambulika katika utafiti huu kama sihiri.

Kwa ujumla, wimbo umetumika kama mbinu ya kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa matendo mbalimbali ya kisihiri yamewasilishwa kupitia wimbo. Wimbo husika huwa na maneno maalumu ambayo hutumika kama masharti katika kukamilisha matendo fulani ya kisihiri. Licha ya hayo, zipo nyimbo ambazo huimbwa na msihiri kadiri anavyosukumwa kuimba bila kuzingatia maneno maalumu. Pia, utafiti wa makala hii umebaini kuwa nyimbo za kisihiri huhusisha nguvu isiyo ya kawaida katika kukamilisha masuala mbalimbali. Nguvu husika hutoka kwa Mungu, wahenga, majitu, majini na mazimwi (Florian, 2016). Austern (1990) anaeleza kuwa msihiri kabla ya kuimba huanza kwa kuwasifu miungu na roho mbalimbali zenye nguvu lakini

zisizoonekana. Kutokana na hayo, makala hii imeeleza bayana kwa kutumia mifano kutoka katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto jinsi wimbo ulivyotumika kisihiri kusababisha kiti kilichokaliwa na mtu kupaa angani.

5.5 Namna ya Utendaji

Utendaji ni ufanikishaji au uwasilishaji wa suala fulani kwa matendo (Sabherwal na Jeyaraj, 2015). Utendaji huhusisha uchezeshaji wa viungo mbalimbali vya mwili kama vile mikono, kichwa na hata miguu wakati wa kuwasilisha jambo fulani kwa hadhira (Mulokozi, 1996). Kutokana na maelezo ya wataalamu tajwa hapo juu, ni kwamba ili utendaji uwepo ni lazima viungo mbalimbali vya mwili wa fanani vitumike. Mulokozi anafafanua zaidi kuwa utendaji hukamilika kwa msaada wa vitu mbalimbali kama vile fimbo, vifaa vyenye ncha kali au makali na hata maleba maalumu. Aidha, mbinu ya namna au jinsi ya utendaji imetumika katika kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Mbinu hii imegawanyika katika makundi mbalimbali kama vile kutenda kwa kugusa na kutemea mate. Mathalani, mbinu ya kugusa imetumika katika bunilizi ya *Sinderela* wakati Bibi Sinderela akibadilisha maumbo ya vitu mbalimbali kuwa vile anavyovitaka kwa kuvigusa. Data kutoka katika bunilizi ya *Sinderela* inathibitisha haya pale mwandishi anapoeleza:

> “Bibi Sinderela akaligusa tikiti likawa gari zuri, panya wanageuka kuwa farasi wa kulivuta gari, punda kuwa dereva wa gari na mbwa akawa mlinzi. Bibi akamgusa Sinderela begani na nguo alizozivaa zikabadilika na kuwa nguo nzuri zinazometameta. Miguuni alivaa viatu vizuri vya kioo vilivyometameta” (Moshi, 1995: 12-13).

Dondoo hilo linaonesha namna vitu mbalimbali vilivyobadilika maumbo yake baada ya kuguswa na bibi Sinderela. Kugusa ni kupapasa kitu au kiungo cha mwili kwa wepesi (BAKITA, 2022). Kutokana na hayo, kugusa hakuna uhusiano wowote na mabadiliko ya kitu au mtu. Aidha, madondoo ya makala hii yameonesha kuwa vitu mbalimbali vimeguswa na kubadilika kutoka katika maumbo yake asilia na kuchukua sura na maumbile ya vitu vingine. Suala hili linashangaza sana na kuthibitisha kuwa bibi Sinderela alikuwa na nguvu zisizo za kawaida katika kutekeleza masuala aliyoyafanya kwa kugusa. Nguvu hiyo ndiyo iliyobadilisha mambo yote tajwa hapo juu. Pia, imebainika kuwa ili vitu au watu waweze kubadilika ni lazima waguswe. Kwa kugusa, sihiri ya bibi Sinderela ilivibadili vitu na viumbe mbalimbali kuwa na mwonekano wa vitu alivyovihitaji. Kwa mfano, data inaonesha kuwa tikiti liliguswa na kuwa gari zuri. Kiuhalisia, tikiki ni tunda jamii ya tango ambalo ni kubwa na linapoiva ndani huwa jekundu (BAKITA, 2022). Gari ni chombo kinachotumika kwa ajili ya usafiri wa ardhini kumtoa mtu na mali zake kutoka eneo moja kwenda jingine (Paterson, 2000). Kutokana na hayo, tikiti haliwezi kuwa gari. Ili suala kama hilo lifanyike ni lazima ihusishwe nguvu isiyo ya kawaida ambayo katika makala hii inarejelewa kama sihiri.

Samwel (2012) anaeleza kuwa sihiri huweza kutoka kwa wahenga na husaidia kukamilisha masuala mbalimbali kwa namna isiyo ya kawaida. Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa Bibi Sinderela alitumika kubeba sihiri kutoka kwa wahenga wa jamii ya kina Sinderela. Pia, imebainika kuwa lengo la Bibi Sinderela lilikuwa ni kutoa msaada kwa mtu wa damu yake ambaye ni mjukuu wake, Sinderela. Maelezo hayo yanaonesha kuwa wahenga hutumika kama roho za siri na huwa na nguvu kubwa inayoweza kuwasaidia watu katika kutatua matatizo yao (Faraone, 2011). Aidha, makala hii imebaini kuwa Sinderela aliweza kutatua matatizo yake kutokana na msaada alioupata kutoka kwa wahenga kupitia bibi yake aliyekuwa marehemu. Aidha, tikiti, panya, nguo na punda ni vitu na wanyama halisi wanaopatikana katika mazingira halisi. Suala lisiloaminika ni nguo kuukuu kuguswa na kubadilika kuwa nguo mpya na nzuri, tikiti kuwa gari pamoja na panya kuwa farasi. Masuala hayo kwa pamoja hayawezi kutekelezeka bila kuhusisha sihiri. Hivyo, mbinu ya kugusa hutumika kuwasilisha usihiri wa masuala mbalimbali kama ilivyobainika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Pia, mbinu ya utendaji wa kutemea mate na kusugua imetumika kuwasilisha matendo ya kisihiri katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua*, na Ali-Gombe katika harakati za kutaka kumfufua kaka yake Ali-Simba aliyeuawa kwa hujuma na askari wa Mfalme Daudi. Mate ni kiowevu kinachozalishwa na tezi ndani ya kinywa ili kukiweka kinywa katika hali ya unyevu, kukiwezesha kuonja, kutafuna na kumeza chakula tumboni kwa ajili ya kumeng'enywa (BAKITA, 2022). BAKITA linafafanua kuwa kusugua ni kupaka, kupapasa au kusogeza kufanya kitu juu ya kingine kwa nguvu na kwa kurudiarudia ili kukiondolea uchafu, kuking'arisha au kukifanya kuwa laini. Kutokana na hayo, matendo mawili yaliyoelezwa hapo juu (kutemea mate na kusugua) hayana uhusiano wowote. Aidha, bunilizi za makala hii zimeonesha usihiri wa kutemea mate na kusugua kumfufua mtu ambaye ni Ali-Simba. Data kutoka katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* inabainisha haya mwandishi anapoeleza:

> Ali-Gombe alipofika kwa mfalme Daudi aliomba kuoneshwa mahali alipozikwa Ali-Simba. Alifukua kaburi na kumtoa kaka yake Ali-Simba. Alimtemea mate mara tatu utosini na kuanza kumsugua taratibu kwa kutumia unga wa maini ya baba yake aliokuwa nao. Robo saa baadaye, Ali-Simba alisimama akamkumbatia nduguye huku machozi yakimtoka (Mzindakaya, 2005: 41).

Dondoo hilo linaonesha namna Ali-Gombe alivyomfufua kaka yake Ali-Simba kwa kumtemea mate utosini na kumsugua. Yote hayo yaliwezekana kwa sababu Ali-Gombe alikuwa na sihiri ya unga wa maini ya baba yake uliomwezesha kukamilisha hayo. Pia, maelezo ya dondoo hapo juu yanashabihiana na yale ya Akima (1982) anayeeleza kuwa mizimu husaidia watu kutatua changamoto zao za maisha kupitia watu wa karibu nao au wao wenyewe. Hivyo, Ali-Gombe alitumia unga wa maini ya baba yake aliyekuwa marehemu kumrudishia uhai kaka yake

Ali-Simba. Aidha, kitendo cha kutema mate na kusugua ni halisi na hufanywa mara kwa mara na watu katika jamii. Suala ambalo halijazoeleka ni mtu kurudishiwa uhai (kufufuliwa) baada ya kufa na kuzikwa kwa kutemewa mate na kusuguliwa utosini. Tendo hili linadhihirisha kuwa kutemewa mate na kusuguliwa utosini ni miongoni mwa mbinu zilizowasilisha usihiri wa masuala mbalimbali katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto.

6.0 Hitimisho

Makala hii imemakinikia mbinu zinazosawiri usihiri katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Mjadala umeongozwa na Nadharia ya Uhalisiajabu. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa kuna mbinu mbalimbali zinazosawiri usihiri katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu ya ndoto, mbinu ya utamkaji wa maneno, mbinu ya wimbo, mbinu ya ukiukaji wa masharti na mbinu ya namna ya utendaji. Kupitia mbinu hizo, usihiri wa masuala mbalimbali kama vile mtu kufufuliwa kwa kutemewa mate kichwani na kusuguliwa, vitu kubadilika maumbo yake ya asili, kwa mfano, tikiti kuwa gari kwa kuguswa, watu kuhamishwa kutoka eneo moja kwenda jingine kwa utamkaji wa maneno, funga na fungua macho, mtu kuyeyuka baada ya kukiuka masharti ya kutokula nyama ya fahali pamoja na wimbo kuwezesha kiti kilichokaliwa na mtu kupaa hewani na kumfikisha mtu husika mawinguni. Aidha, mbinu husika zimeonesha mfungamano mkubwa kati ya masuala halisi na yale yasiyo halisi, hivyo, kufikisha ujumbe wa mwandishi kwa hadhira kama ilivyokusudiwa na mwandishi. Makala hii inachangia katika taaluma ya fasihi kwa kuonesha kuwa sihiri ni kipengele muhimu cha kisanaa katika utunzi wa kazi mbalimbali za kifasihi kwani imepanua kipengele cha sihiri kwa kueleza mbinu anuwai zinazotumika katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya kisihiri katika fasihi hususani katika bunilizi za fasihi ya Kiswahili za watoto.

Marejeleo

Abercromby, J. (1990) “Magic Songs of the Finns”. *Folklore,* Juz.1:17- 46. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/1253688. Imesomwa tarehe 10 Mei 2024.

Akima, T. (1982) “The Songs of the Dead: Poetry, Drama, and Ancient Death Rituals of Japan”. *The Journal of Asian Studies*, Juz. 41(3): 485-509. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/2055245. Ilisomwa tarehe 25/3/2023.

Anne, C.H. (1994) *Lies that Tell the Truth: Magic Realism Seen Through Contemporary Fiction From Britain*. New York: Amsterdam.

Annus, M. (2015) “Magic and Feminity Power in Medieval Literature”. *Literature,* Juz. 293:1-20. Inapatikana katika https://dc.etsu.edu/honors. Ilisomwa tarehe 27 Desemba 2022.

Austern, A.E. (1990). "Sexless Spirits? Gender Ideology and Dryden's Musical Magic." *The Musical Quarterly*, Juz. 93(2): 297-328. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/40783238. Ilisomwa tarehe 20 Juni 2014.

BAKITA (2022) *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la 3). LONGHORN.

Bakize, L.H. (2012) "Fantansia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto". *Kioo cha Lugha*, Juz. 8: 122-134.

Barley, M.D. (2006) "The Meaning of Magic". *Magic Rituals and Witchcraft*, Juz. 1(1): 1-23. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/24767701. Ilisomwa tarehe 7 Desemba 2022.

Bowers, M.A. (2004) *Magic(al) Realism*. New York: Routledge 2Park Squire, Milton Park, Abingdon, Oxon OX14 4RN.

Bradley, K. (1997) "Law, Magic, and Culture in the Apologia of Apuleius". *Phoenix*, Juz. 51(2): 203-223. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/1088495. Ilisomwa tarehe 26 Machi 2023.

Brock-Utne, B. (2018) "Researching Language and Culture in Africa Uusing an Autoethnographic Approach". *International Review of Education*, Juz. 64(6): 713-735. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/44980159. Ilisomwa tarehe 08 Machi 2024.

Cahill, M. (2012) "The Role of Magic in Fantasy Literature: Exposing Reality through Fantancy". *English*, Juz. 8: 1 - 44. Inapatikana katika https://scholarsarchive. library.albany.edu/honors .com. Ilisomwa tarehe 12 Novemba 2021.

Capers, B. (2006) "On Andy Warhol's "Electric Chair". *California Law Review*, Juz. 94(1): 243-260. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/20439032. Ilisomwa tarehe 16 Februari 2024.

Cooper, B. (1998) *Magical Realism in West African Fiction*. New York: Routledge.

Dimmock, M. na Fisher, A. (2017) "Eating Animals. In *Ethics for A-Level* (1st ed., pp. 219-234). Open Book Publishers. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/j.ctt1wc7r6j.18. Ilisomwa tarehe 05 Februari 2017.

Evans, W.E., Milanak, B.M. na Rose, J.L. (2002) "Magical Beliefs and Ritual in Young Children." *Child Psychiatry and Human Development*, Juz. 33(1): 43-58. Inapatikana katika https://www.researchgate.net/publication /11187693. Ilisomwa tarehe 06 Machi 2022.

Faraone, C.A. (2011) "Magical and Medical Approaches to the Wandering Womb in the Ancient Greek World". *Classical Antiquity*, Juz. 30(1): 1-32. Inapatikana katika https://doi.org/10.1525/ca.2011.30.1.1. Ilisomwa tarehe 16/10/2023.

Faris, B.W. (2004) *Ordinary Enchantment Magical Realism and the Remistification of Arrative.* Nashville: Vanderbilt UP.

Fish, A. (2016) "Making Afro-Urban Magic". *Transition*, Juz. 121:70-80. Inapatikana katika https://doi.org/10.2979/transition. Ilisomwa tarehe 22 Machi 2023.

Florian, E.R. (2016) "Thunder Magic Ritual and Thunder Divinities." *Asian Humanities*, Juz. 1: 9-18. Inapatikana katika https://hdl.handle.net/2324 /1654565. Ilisomwa tarehe 03 Februari 2022.

Fox, J. (2006) *What Books About Magic do for Children-that Others Stories Can't.* Oxford Children's Books. Inapatikana katika https:/www.readbrightly .com. Ilisomwa tarehe 04 Juni 2022.

Fukkink, R.G. na de Glopper, K. (1998) "Effects of Instruction in Deriving Word Meaning from Context: A Meta-Analysis". *Review of Educational Research*, Juz. 68(4):450-469. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307 /1170735. Ilisosomwa tarehe 13 Juni 2023.

Gavin, L.M. (2021) The Magic of Play: How it Inpires and Aids Early Development. Kidshealth. Inapatikana katika https://kidshealth.org /en/parents/play-magic.html. Imesomwa tarehe 10 Desemba 2022.

Haward, V. (2003) "A Real's Mans Ring." *Gender and the Invection*, Juz. 36 (4):837-856. Inapatikana katika https://www.org.Jstors/stable/3790353. Ilisomwa tarehe 15 Mei 2022.

Kimaryo, J. (2008). Religious Rituals and the Symbolic Use of Vessels in African Traditional Ceremonies. Nairobi: University of Nairobi Press. Inapatikana katika https://doi.org/10.1890/0012-9623. Imesomwa tarehe 08 Juni 2023.

Kohnert, D. (1996) "On the Renaissance of African Modes of Thought-The Example of the Belief in Magic and Witchcraft". *Munich Personal RePEc Archive* (MPRA), Juz. 7019: 33-54. Inapatikana katika https://mpra.ub.uni-muenchen.de/7019/. Ilisomwa tarehe 05 Januari 2022.

Kozlov, M.V. (2003) "Pseudoreplication in Russian Ecological Publications". *Bulletin of the Ecological Society of America*, Juz. 84(1): 45-47. Inapatikana katika https://doi.org/10.1890/0012-9623. Ilisomwa tarehe 22 Februari 2024.

Lawrence, S.E. (2015) "Witchcraft, Sorcery, Violence: Matrilineal and Decolonial Reflections". Katika M. Forsyth na R. Eves (Wah.), *Talking it Through: Responses to Sorcery and Witchcraft Beliefs and Practices in Melanesia*. ANU Press. Kur. 55-74. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/j.ctt169wd7b.7. Ilisomwa tarehe 11 Desemba 2022.

Mahmood, W.S. (2020) "Fantasy in Children Literature." *Journal of Arts, Literature, Humanities and Social Sciences*, Juz. 59: 452-465. Inapatikana katika www.Jalhass.com. Imesomwa tarehe 30 Oktoba 2022.

Mariki, F. (2004) *Hadithi ya Morile*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Mbiti, J.S. (1957) *African Religions & Philosophy.* Nairobi: East African Education Publishers.

Meilinger, P.S. (2000) "The Historiography of Airpower: Theory and Doctrine". *The Journal of Military History*, Juz. 64(2): 467-501. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/120248. Ilisomwa tarehe 13 Mei 2023.

Moshi, R. (1995) *Sinderela.* Dar es Salaam: Mture Publishers Limited.

Mulokozi, M.M. (1996) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M.M. (2002) *The African Epic Contraverssy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers

Mzindakaya, C. (2005) *Hadithi za Kusisimua*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.

Ngugi, P.M, Lyimo, E.B na Bakize, L.H. (2019) *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Nlya, L. (2021) "Magic and Fantasy: Why Children are Drown to Fiction". *KIDPRESSROOM*, Juz. 3: 20-30. Inapatikana katika https:/www.kidpressroom.com. Ilisomwa tarehe 05 Agosti 2022.

Owen. D. (2012) *Magic: A Very Short Introduction*. New York: Oxford University Press.

Paterson, M. (2000) "Car Culture and Global Environmental Politics". *Review of International Studies*, Juz. 26(2): 253-270. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/20097673. Ilisomwa tarehe 08 Machi 2024.

Pfeffer, W.T. (2011) "Land Ice and Sea Level Rise: A Thirty-Year Perspective". *Oceanography*, Juz. 24(2): 94-111. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/24861271. Ilisomwa tarehe 07 Mei 2022.

Sabherwal, R. na Jeyaraj, A. (2015) "Information Technology Impacts on Firm Performance: An Extension of Kohli and Devaraj (2003)" *MIS Quarterly*, Juz. 39(4): 809-836. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/ 26628653. Ilisomwa tarehe 14 Juni 2023.

Salsich, P.W. (2012) "Homeownership-Dream or Disaster?" *Journal of Affordable Housing & Community Development Law*, Juz. 21(1): 17-71. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/24389815. Imesomwa tarehe 08 Januari 2024.

Samwel, M. (2012) *Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na Bongo Fleva.* Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Sharma, V. (2018). The Principles of Magical Practice: An analysis. New Delhi: Mystic Publishers. Inapatikana katika https:/www.kidpressroom.com. Imesomwa tarehe 07 Februari 2024.

Simpkins, S. (1988) "Magical Strategies: The Supplement of Realism". *Twentieth Century Literature*, Juz. 34(2):140-154. Duke University Press. Inapatikana katika *https://www.jstors.org/stable/441074*. Ilisomwa tarehe 10 Septemba 2022.

Slaughter, V., Heron, M., Jenkins, L., Tilse, E., Müller, U. na Liebermann, D. (2004) "Origins and Early Development of Human Body Knowledge". *Monographs of the Society for Research in Child Development*, Juz. 69(2): 51-113. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/3701402. Ilisomwa tarehe 12 Januari 2024.

Sommer, S. R. (2001) "C'mon to My House": Underground-House Dancing". *Dance Research Journal*, Juz. 33(2): 72-86. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/1477805. Ilisomwa tarehe 12 Februari 2024.

Stolz, R. (2018) "Spirits Follow the Words: Stories as Spirit Traces among the Khmu of Northern Laos. Social Analysis: *The International Journal of Anthropology*, Juz. 62(3): 109-127. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/26952423. Ilisomwa tarehe 02 Januari 2023.

Subbortsky, E. (2010) *Mechanism, Function and Development of Magic Thinking and Behaviour*. Oxford University Press: New York. Inapatikana katika https://www.researchgat.net/publication/261595945. Ilisomwa Tarehe 18 Oktoba 2022.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Varelius, J. (2013) "Ending Life, Morality, and Meaning". *Ethical Theory and Moral Practice*, Juz. 16(3):559-574. Inapatikana katika http://www .jstor.org/stable/24478619. Ilisomwa tarehe 7 Novemba 2023.

Wafula, R.M. na Kimani, N. (2007) Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Publisher.

Weismantel, M. (2004) "Moche Sex Pots: Reproduction and Temporality in Ancient South America". *American Anthropologist*, Juz. 106 (3): 495-505. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/3567614. Ilisomwa tarehe 08 Desemba 2023.

Zuesse, E. M. (1975) "Divination and Deity in African Religion". *History of Religion*, Juz. 15(2): 158-182. Inapatikana katika http://www.jstor.org /stable/ 1061929. Ilisomwa tarehe 06 Novemba 2022.